**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**015/1**

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2** **Jumatano, 09 Novemba 2016 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote.**
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.


KM-2016

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU A (Alama 10)
## SUNNAH NA HADITHI

1. Katika kipengele (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha **andika herufi yake** katika kijitabu chako c kujibia.

(i) Ni ipi kati ya aya hizi zifuatazo inaeleza umuhimu wa kufuata Sunnah ya Mtume (s.a.w)?
A Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni; Mwenyezi Mung atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu …" (3:31).
B Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila Wahiy (ufunuo), uliofunuliwa (kwake). (53:3-4).
C "Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho …" (33: 21).
D … Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. N muogopeni Mwenyezi Mungu; kwa yakini Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu (59:7).
E Enyi mlioamini! "Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume, wala msiviharibu vitendo vyenu" (47.33).

(ii) Moja ya kauli zifuatazo ni mtazamo potofu juu ya Sunnah za Mtume (s.a.w):
A Sunnah ni mwenendo wa Mtume (s.a.w).
B Sunnah ndio tafsiri ya Qur'an katika utekelezaji wa Uislamu.
C Sunnah ni tafsiri ya maagizo ya Allah (s.w) katika utendaji wa kila siku.
D Sunnah ya Mtume (s.a.w) ndio njia ya kumfikisha kwenye radhi za Allah (s.w).
E Sunnah ni matendo aliyofanya Mtume (s.a.w) ambayo Muislamu ana hiari ya kuyaiga au kutoyaiga.

(iii) Mtume (s.a.w) amesema kwamba mtu anapofariki dunia hukatika amali zake isipokuwa mambo matatu, ambayo ni
A Kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Salat Tahajudi, Elimu yenye manufaa
B Salat Tahajudi, Elimu yenye manufaa, mtoto mwema atakayemuombea dua
C Elimu yenye manufaa, sadaqat yenye kuendelea, mtoto mwema atakayemuombea dua
D Ibada ya Hija na Umra, sadaqat yenye kuendelea, mtoto mwema atakayemuombea dua
E Sala ya Tarawekh, Elimu yenye manufaa, mtoto mwema atakayemuombea dua.

(iv) Hadithi ya daraja la kwanza kwa usahihi inapatikana katika kitabu kipi?
A Al – Muwatta.
B Sahih Bukhari
C Sahih Bukhari na Sahih Muslim
D Sahih Muslim.
E Sunan Abu Daud na Sahih Muslim.

(v) Ni tukio lipi lililotokea kipindi cha Maswahaba na kuufanya uandishi wa Hadithi kuwa muhimu?
A Kutawafu kwa Mtume (s.a.w).
B Kuzuka kwa vita.
C Kupanuka kwa Dola ya Kiislamu.
D Kuzuka kwa Hadithi za Uongo.
E Kutoweka kwa maswahaba wa Mtume.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(vi) Hadithi inayomzulia Mtume (s.a.w) huitwa

A Ahad
B Dhaifu
C Riwaya
D Hasan
E Maudhui

(vii) Hadithi na Sunnah za Mtume wakati wa Mtume zilihifadhiwa zaidi katika

A matendo na katika nyoyo
B magamba ya mitende
C maandishi na katika nyoyo
D vitabu vya mwanzo vya Hadithi
E maandishi na matendo.

(viii) Katika vipindi vifuatavyo, ni kipindi kipi hapakushuhudiwa kitabu chochote cha Hadithi?

A 11 H - 100 H.
B 101 H - 200 H
C 1 H - 10 H
D 201 H - 300 H
E 301 H - 400 H.

(ix) Kitabu cha kwanza cha Hadithi za Mtume (s.a.w) kilichopangwa vizuri na hivyo kutegemewa na Ummah wa Waislamu kipindi cha Tabiina ni

A Alqatadaya
B Juzuu ya Ibn Abbas
C Masnad ya Ibn Hambal
D Al-muwatta
E Sahih ya Bukhari.

(x) "Na anachokupeni Mtume (s.a.w) basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho" (59:7). Tunajifunza nini kutokana na aya hii?

A Katika Uislamu ni marufuku watu kuingiza rai zao.
B Hakuna hiari kufuata mafundisho ya Mtume (s.a.w).
C Allah (s.w) yuko na Mtume wake muda wote.
D Qur'an inatoka kwa Allah (s.w) kupitia kwa Mtume (s.a.w).
E Chanzo cha dini ya Kiislamu ni Mtume (s.a.w).



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

**SEHEMU B (Alama 15)**
**QUR-AN**

2. Oanisha aya za Qur'an zilizopo katika **Orodha A** na maelezo ya aya hizo yaliyopo katika **Orodha B**. Andika herufi sahihi pembeni ya namba kutoka orodha A katika kijitabu chako cha kujibia.

| | **Orodha A** | | **Orodha B** |
|---|---|---|---|
| (i) | "Kwa jina la Allah mwingi wa rehma mwenye kurehemu. … Njia ya wale uliowaneemesha, na sio ya wale waliokasirikiwa wala ya wale waliopotea" (1:1-7). | A | Qur'an ni ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. |
| (ii) | "Na haikuwa kwa mtu kwamba Allah anasema nae ila kwa Ilham au nyuma ya pazia, au hutuma mjumbe nae humfunulia kiasi anachotaka" (42:51). | B | Sura ya tano kushuka na pia ni sura ya kwanza kushuka nzima. |
| (iii) | "Je! Wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wasiojua? …" (39:9) | C | Mwanadamu anatakiwa avitumie vizuri vipawa alivyojaaliwa. |
| (iv) | "Ni mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa Qur'an ili uwe mwongozo kwa watu" (2:185). | D | Athari ya kutenda maovu. |
| (v) | "Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma" (111:2). | E | Mwenyezi Mungu anavyowasiliana na viumbe wake. |
| (vi) | "Na kaeni majumbani mwenu wala msioneshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionesha mapambo yao wanawake wa zama za ujahili…" (33:33). | F | Mafanikio ya Waislamu yamo ndani ya katiba yao. |
| (vii) | Suratul Ikhlas kuanzia aya ya kwanza hadi ya nne. (112:1-4). | G | Amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w). |
| (viii) | "Lakini Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapokuja ajali yake; na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda (yote)". (63:11). | H | Elimu ina nafasi ya kwanza katika Uislamu. |
| (ix) | "Bila shaka tumemuumba mwanadamu kwa umbo lililo bora kabisa. Halafu tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini" (95:4 – 5). | I | Hijaab katika Uislamu. |
| (x) | "Usitikise ulimi wako kwa (Kuufanyia haraka) Wahiy kwa hakika ni juu yetu kuukusanya na kuusomesha" (75:16 – 17). | J | Mwenyezi Mungu ni mpweke, hana mwanzo wala mwisho. |
| (xi) | "Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake. Ni Uongozi kwa wamchao Allah" (2:2). | K | Abuu Lahab. |
| (xii) | "Basi kwa hakika baada ya dhiki (huja) faraja". (94:5). | L | Laana ya Mwenyezi Mungu iko juu ya wale wanaokanusha Uislamu na kuupiga vita kwa kibri na jeuri. |
| (xiii) | "Ila wale walioamini na wakafanya mema. Wakausiana haki na wakausiana kushikamana na subira" (103:3). | M | Imani ya kweli huambatana na vitendo vizuri. |
| (xiv) | "… Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi)" (6:116). | N | Uislamu sio dini ya ubinafsi, Waislamu ni lazima wasimamishe haki na uadilifu katika jamii. |
| (xv) | "Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mmezitumiaje)" (102 :8). | O | Wakati ni rasilimali muhimu inayotakiwa itumiwe kwa uangalifu mkubwa. |
| | | P | Usiku wenye cheo. |
| | | Q | Mwenyezi Mungu huapia viumbe vyake. |
| | | R | Mafanikio huja baada ya kufanya juhudi kwa kadiri ya uwezo wa kibinadamu. |
| | | S | Qur'an haitawaongoza makafiri. |
| | | T | Lengo la Qur'an. |



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU C (Alama 15)
## TAWHIID

3. Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika **herufi na namba tu** zinazohusika katika Kitabu chako cha kujibia.

(a) Mtiririko sahihi wa nguzo za Uislamu kisha za Imani ni kama ifuatavyo:
- (i) Kuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake.
- (ii) Kuamini siku ya mwisho na kudra zake.
- (iii) Kushuhudia Allah na kuwa Muhammad ni Mtume wake.
- (iv) Kuamini Vitabu vya Allah (s.w) na Mitume wake.
- (v) Kusimamisha swala, kutoa zaka, kufunga mwezi wa Ramadhani na kuhiji Makka.

(b) Mwenyezi Mungu anawaahidi wanaokana ufufuo kwa kuwaambia katika Qur'an (16:38-40):
- (i) (Atawafufua) ili kuwabainishia yale waliyohitilafiana.
- (ii) Kwa nini (asiwafufue)? Ni ahadi iliyolazimika kwake (kuwafufua na kuwalipa).
- (iii) Lakini watu wengi hawajui.
- (iv) Nao (wakaapa) kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa kiapo chao cha nguvu (kwamba) hatawafufua wafao.
- (v) Na ili wajue waliokufuru ya kwamba wao ni waongo.

(c) "Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adam) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeliane)… " (49:13).
Kutokana na aya hii tunafahamishwa kwamba:
- (i) Mwenyezi Mungu amewaweka watu katika mataifa mbalimbali na tofauti.
- (ii) Mwenyezi Mungu amefanya mambo kwa elimu yake kwani yeye ni mjuzi wa habari zote.
- (iii) Mtu bora kwa watu ni yule amchaye Mwenyezi Mungu zaidi.
- (iv) Mwenyezi Mungu ameumba watu wote kutokana na Adamu na Hawa.
- (v) Mwenyezi Mungu amefanya hivyo ili watu wajuane tu si wadharauliane.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D (Alama 30)
## FIQH

4. Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi kwa **kuandika majibu yako** katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Ainisha mambo mawili ambayo kwayo muumini huhifadhi swala.

(b) Fafanua mambo mawili ya kuzingatia zaidi unaposafisha paliponajisika kwa kinyesi cha kuku.

(c) Bainisha vitu viwili ambavyo katika swala ya maiti ni nguzo lakini havipatikani katika swala ya kawaida.

(d) Utoaji wa Zaka na Sadaqa utafikia lengo iwapo mtoaji atajiepusha na mambo manne. Taja mambo hayo.

(e) Taja Nissabu ya Dhahabu na ya pesa Taslim.

(f) Andika tafsiri ya aya ya Qur'an inayobainisha kufaradhishwa kwa funga.

(g) Andika maana ya swaumu kisheria na kisha bainisha lengo la swaumu.

(h) Bainisha makundi manne tu ya Waislamu ambao hawalazimiki kufunga mwezi wa Ramadhani.

(i) Orodhesha faida kuu mbili miongoni mwa faida zitokanazo na utekelezaji wa Ibada ya Hija.

(j) Ainisha masharti manne ya Kutufu.

(k) Taja mambo manne ambayo mwenye kuhiji Hija ya Qiran analazimika kufanya.

(l) Ainisha masharti manne yanayomfanya mwanamke wa kiislamu asiruhusiwe kufunga ndoa.

(m) Fafanua hekima mbili za sheria ya mwanamke kukaa Eda ya kuachwa.

(n) Fafanua masharti mawili yanayomwezesha mtu kurithi.

(o) Taja mambo mawili yanayozuia urithi katika sheria ya kiislamu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU E (Alama 30)
## TAREKH

5. Chagua **neno au kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe sentensi (a) – (o) **kwa kuandika majibu sahihi tu** katika kijitabu chako cha kujibia. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(i) Hamza
(ii) Jabal Safaa
(iii) Taif
(iv) Chokochoko
(v) Kumuunga mkono
(vi) Mkataba wa Hudaibia
(vii) Madina
(viii) Abuu Jandal
(ix) Asma
(x) Uislamu
(xi) Vitisho
(xii) Nuhu
(xiii) Vita vya Badri
(xiv) Abuu Ayub
(xv) Adam
(xvi) Kumtii Allah na Mtume wake
(xvii) Sarah
(xviii) Abu Lahabi
(xix) Mus'ab bin Umayr
(xx) Bibi Khadija
(xxi) Utume
(xxii) Hajir
(xxiii) Uhudi
(xxiv) Ghar-thaur
(xxv) Waraqa bin Naufal
(xxvi) Vita vya Ahzab
(xxvii) Alipoumbwa
(xxviii) Kurubuni
(xxix) Abuu Bakar
(xxx) Kumwezesha kukubalika

**Maswali**

(a) Mtume alipopewa amri ya kulingania Jahara alipanda __________ katika mkusanyiko huo alikuwapo ami yake __________.

(b) Mauaji ya __________ katika vita vya __________ yalikuwa ya kikatili.

(c) __________ ndiye aliyewahudumia Mtume na Abuu Bakari katika __________ mara tu baada ya kutoka nyumbani kwao.

(d) Mtume wa pili baada ya __________ ni __________.

(e) Baada ya makubaliano ya Aqaba, Mtume (s.a.w) alimtuma __________ kwenda __________ kufundisha Uislamu.

(f) Baada ya kumsimulia mkewe __________ alipeleka ujumbe kwa ______ ambaye ni jamaa yake.

(g) __________ ndiye alikuwa wa kwanza __________ mtume kwa kila analosema Mtume.

(h) __________alisilimu baada ya kutiwa saini __________.

(i) Mtume alipofika __________ alifikia katika nyumba ya __________.

(j) Katika __________ makundi mengi yaliungana dhidi ya __________.

(k) Miongoni mwa mbinu za Makureishi katika kuupiga vita Uislamu ni ________ na ________.

(l) ________ ni matokeo ya ________ za makafiri wa kikuraish dhidi ya dola ya Kiislamu.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

(m) Mama ___________ na ___________ walikuwa wake wa Nabii Ibrahim.

(n) Kazi ya msingi iliyofanywa na mafunzo ya kiilhamu kwa Mtume kabla ya kupewa _________ ni __________.

(o) Funzo kubwa kutokana na vita vya _________ ni kuwa hapana mafanikio bila ya ___________.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner